## 21:1-24:25 MAMBO MENGINE

Mwandishi wa kitabu cha pili cha Samweli amemaliza ripoti ya historia ya utawala wa Daudi. Baada ya habari za dhambi ya Daudi na Bathsheba, mwandishi alishughulika zaidi kuonyesha jinsi tendo lile moja lilivyobadilisha maendeleo ya maisha ya Daudi. Sasa anarudia kueleza habari mbalimbali na kuandika nyimbo zinazoonyesha matatizo mengine yaliyompata Daudi wakati wa utawala wake na jinsi Mungu alivyomlinda na kumsaidia katika matatizo hayo. (Habari za miaka ya mwisho ya maisha ya Daudi zimeandikwa katika mafungu ya kwanza ya kitabu cha kwanza cha Wafalme.)

### Hukumu na haki (21:1-22)

Tatizo mojawapo la Daudi lilikuwa shida ya njaa ya miaka mitatu katika nchi nzima. Mungu alimwonyesha kwamba njaa hiyo ilikuwa hukumu yake juu ya Israeli, kwa sababu Sauli aliwaua Wagibeoni, na hivyo alivunja kiapo ambacho Yoshua, mjumbe wa taifa lote, aliwaapia Wagibeoni katika jina la Mungu (21:1-2; taz. Yos 9:15,19-21). Dhambi ya Sauli ilibidi kusafishwa, na madai ya Wagibeoni yalipaswa kuridhishwa. Kwa hiyo watu saba wa wazao wa Sauli waliuawa, idadi hiyo ikiwa mfano wa ridhaa kamili (3-9).

Daudi alishikwa na huruma alipomwona suria mmoja wa zamani wa Sauli akimsikitikia mume wake aliyekufa. Hivyo alijaribu kumfariji, akipanga mazishi ya heshima kwa mifupa ya Sauli na Yonathani. Labda mifupa hiyo ilizikwa karibu na maid ya Wabenyamini saba waliohukumiwa kifo. Jambo hili pia lilionyesha kwamba Daudi mwenyewe hakuwa na kisa juu ya mfalme wa zamani, bali aliwaua watu wale saba kwa sababu ya agizo la Mungu tu la kudai haki. Baada ya hayo Mungu aliondoa hukumu yake juu ya Israeli kwa kudhibiti njaa nchini (10-14).

Wakati wa vita fulani kati ya Wafilisti na Waisraeli, jitu mmoja wa Wafilisti aliyeonekana kama alitaka kulipiza kisasi kwa ajili ya Goliathi, akijaribu kumwua Daudi. Lakini jitu mwenyewe aliuawa na askari hodari mmoja wa Daudi (15-17). Majitu wengine watatu wa Wafilisti waliuawa na Waisraeli katika matukio mbalimbali (18-22; taz.lNya 20:5).

### Zaburi mbili (22:1-23:7)

Zaburi ya kwanza katika hizo ilitungwa na Daudi ili kuadhimisha ushindi wake juu ya maadui zake. Baadaye zaburi hiyo ilitungiwa sauti za muziki ili itumiwe katika ibada za hekaluni, nayo inaonekana katika kitabu cha Zaburi ikiwa Zaburi ya 18.

Daudi alianza Zaburi yake kwa kumsifu Mungu aliyejibu maombi yake daima na kumwokoa na hatari ya mauti (22:1-7). Mungu alionyesha nguvu zake katika matetemeko ya nchi, upepo, mvua, umeme, ngurumo na giza, na mara nyingine alitumia nguvu hizo ili kumwokoa Daudi kutoka kwa maadui zake (8-20). Mungu alishughulika kwa ajili ya Daudi, kwa sababu ya utii na unyofu wa moyo wake (21-25), akionyesha kwamba anawatendea watu jinsi wanavyostahili (26-30).

Mungu ni mkamilifu katika njia zake zote, kwa hiyo Daudi siku zote aliweza kumtegemea (31-33). Jambo hili lilimlinda Daudi nalo lilimpa uwezo wa kuwa askari na kiongozi wa taifa (34-37), ili aweze kuwashinda maadui zake mara kwa mara (38-43). Sifa zake zilienea mbali sana, na mataifa ya mbali yalijinyenyekeza mbele yake (44-46), lakini yeye alikubali kwa furaha kwamba ukubwa wake wote ulitoka kwa Mungu (47-49). Wafalme wa mbari yake ya baadaye pia wangeweza kuwa na uhakika wa baraka ya Mungu isiyokosa (50-51).

Katika Zaburi yake ya pili, Daudi alitaja kwa kifupi jinsi mfalme aliyemcha Mungu alivyoleta baraka kwa watu wake. Maisha chini ya mfalme wa namna hii yanafananishwa na asubuhi isiyokuwa na mawingu ya mvua. Kama vile jua baada ya mvua linavyosaidia nyasi ili zisitawi, vivyo hivyo mfalme anawafaa watu wake (23:1-4). Nyumba ya mbari ya Daudi ilihakikishiwa baraka ya kudumu, iimarike na kufanikiwa kwa sababu ya agano ambalo Mungu alilifanya na Daudi (5; 7:16). Lakini mfalme mwenye hekima alijua pia kwamba angepaswa kumwadhibu mtu mwovu, naye asingeepuka wajibu wake, ingawa mara nyingi ni vigumu na jambo la hatari kutimiza wajibu huo (6-7).

### Mashujaa wa Daudi (23:8-39)

Kutokana na watu 600 hivi waliokuwa pamoja naye tangu siku zile za ukimbizi wake mbele ya Sauli, Daudi aliteua na kujenga jeshi lenye nguvu sana na lililoaminika kabisa ambalo liliendelea kuwa kiini cha nguvu ya jeshi lake kwa muda wote wa utawala wake wa miaka mingi (taz.lSam 22:1-2; 30:9; 2Sam 2:13,28; 15:18; 18:1-2; 20:7; lNya 11:10). Yoabu alikuwa jemadari wake mkuu (taz.8:16; 20:23).

Chini ya Yoabu walikuwepo mashujaa watatu ambao kila mmojawao alikuwa hodari sana na shujaa wa taifa. Kwa kawaida waliitwa 'Watatu' (8-12; lNya 11:10-14). Baada ya wale 'Watatu' walikuwepo Thelathini', ambao watatu wao walijionyesha zaidi siku moja walipohatarisha maisha yao kwa sababu ya upendo wao kwa Daudi (13-17). Kiongozi wa wale 'Thelathini' alikuwa Abishai, ndugu yake Yoabu. Shujaa mwingine katika wale 'Thelathini' alikuwa Benaya, kiongozi wa kikundi cha kumlinda mfalme binafsi (18-23; taz. maelezo ya 8:18).

Ingawa kundi Hie la mashujaa liliitwa 'Thelathini', idadi ya majina yanayotajwa katika Biblia ni kubwa zaidi kuliko 30. Jambo hili labda lilipatikana kwa sababu orodha ile ilikuwa na majina ya wale waliokufa pamoja na wale walioingia mahali pao (24-39; lNya 11:20-47).

## Sensa ya Daudi na matokeo yake (24:1-25)

Inawezekana kwamba kuongezeka kwa nguvu ya Israeli na kufanikiwa kwao chini ya Daudi kuliwasababisha Daudi na watu wake tabia ya kujisifu, kana kwamba wao, wala siyo Mungu, walikuwa sababu ya ukubwa huo. Mungu aliona kwamba ilifaa kuwaamsha Waisraeli katika dhambi hiyo. Kwa hiyo alimfeli amshawishi Daudi kuchukua sensa ya watu wote. Bila shaka ilikuwa kiburi cha Daudi cha kujisifia katika taifa lake kubwa kilichofanya wazo hilo liwe bora machoni pake, lakini Mungu alitumia tukio hilo ili kudhihirisha kiburi chake na kukiadhibu (24:1-4; lNya 21:1). Maafisa walitekeleza sensa hiyo kwanza mashariki mwa Yordani, kisha kaskazini na baadaye kusini mwa Kanaani (5-9).

Hata kabla Mungu hajaleta hukumu, dhamiri ya Daudi ilimwambia kwamba alikosa. Kwa njia ya nabii, Mungu alimpa Daudi nafasi ya kuchagua moja kati ya maafa matatu ya hukumu, lakini Daudi aliamua kuacha uamuzi wote kwa Mungu na kutegemea neema yake (10-14). Maafa yalitokea katika Israeli, ambayo yalitia udhaifu katika taifa ambalo Daudi alifikiri lilikuwa na afya na nguvu sana. Hata Yerusalemu, jiji ambalo Daudi alijisifia sana, lingaliangamizwa, kama Mungu asingalikomesha maafa yale katika neema yake (15-17).

Ili kuonyesha toba yake, Daudi aliambiwa atoe sadaka kwa BWANA, lakini kwa sababu ya matukio yaliyopita, aliogopa kwenda katika hema la kukutania lililokuwepo Gibeoni (lNya 21:29-30). Kwa hiyo Mungu alimruhusu kubaki Yerusalemu, lakini alimwongoza kununua uwanja wa mlimani kutoka kwa mwenyeji mmoja aliyeitwa Arauna (Ornani). Uwanja huo zamani ulitumiwa na Arauna kwa kupuria nafaka. Daudi alijenga madhabahu katika uwanja huo akamtolea Mungu sadaka (18-20). Arauna alitaka kumpa Daudi uwanja ule kama zawadi, lakini Daudi alitaka kuununua. Kama sadaka yake ilitakiwa kuwa ya maana kwake, lazima atoe gharama kwa ajili yake (21-25).

Baadaye Daudi alinunua eneo lililozunguka uwanja ule pia, akachagua mahali pale pawe uwanja wa kujengea hekalu la Mungu baadaye (lNya pale pale ambapo Ibrahimu alimtoa mwanawe Isaka 21:25; 22:1). Inaonekana kama uwanja ule ulikuwa kuwa sadaka (2Nya 3:1; taz. Mwa 22:2).

### Mfululizo wa miaka tangu Musa mpaka Sulemani

| | |
|---|---|
| 1280 k.K. | Musa awaongoza Waisraeli kutoka Misri; Miaka Jangwani |
| 1240 k.K. | Waisraeli waingia Kanaani chini ya Yoshua; Wakati wa Waamuzi |
| 1050 k.K. | Sauli mfalme wa kwanza katika Israeli |
| 1010 k.K. | Sauli anakufa; Daudi anakuwa mfalme |
| 1003 k.K. | Daudi ateka Yerusalemu |
| 970 k.K. | Daudi anakufa; Sulemani anakuwa mfalme. |

## NYONGEZA

**Ukoo na jamaa wa Daudi**
(Majina ya maana tu; 1Nya 2:11-17)




**Daudi alikuwa na wake na watoto wengi (taz. 2 Sam 5:13)**

Wa maana zaidi ni hawa wafuatao:

| | | |
|---|---|---|
| Mikali | bind Sauli | hakuwa na watoto (ISam 18:27; 2Sam 6:23) |
| Ahinoamu | wa Yezreeli | mama wa Amnoni (ISam 25:43; 2 am 3:2; 13:1) |
| Abigaili | mjane wa Nabali | mama wa Danieli (ISam 25:42; 2Sam 3:3) |
| Maaka | binti wa mfalme wa Geshuri | mama wa Absalomu na Tamari(2Sam 3:3; 13:1,4) |
| Hagithi | | mama wa Adoniya (2Sam 3:4; lFal 1:5) |
| Bathsheba | mke wa zamani wa Uria | mama wa Sulemani na Nathani(2Sam 11:3; 12:24; lNya 3:5; Mt 1:6; Lk 3:31) |